TANZANIA BREWERIES PUBLIC LIMITED COMPANY

MKUTANO MKUU WA 47 WA WANAHISA

KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA AROBAINI NA SABA WA WANAHISA WA KAMPUNI YA TANZANIA BREWERIES PUBLIC LIMITED COMPANY ULIOFANYIKA KWA NJIA YA MTANDAO TAREHE 19 MWEZI AGOSTI, 2020, KUANZIA SAA NNE KAMILI ASUBUHI

WALIOKUWEPO

MH. C. D. MSUYA	: Mwenyekiti
BW. A.B.S. KILEWO	: Mjumbe wa Bodi
BW. L. MUSUSA	: Mjumbe wa Bodi
BW. P. LASWAY	: Mjumbe wa Bodi
BW. P. REDMAN	: Mwakilishi wa ABINBEV AFRICA BV
WAJUMBE WENGINE	: Majina yameambatishwa

WENGINE WALIOHUDHURIA

Bw. HURUMA NTAHENA	: Katibu

WALIOHUDHURIA KWA KUALIKWA

BW. Y. BOMANS	: Mkurugenzi wa Uendelezaji wa Biashara wa TBL
BI. Z. MSIMBE	: Mbia PricewaterhouseCoopers
BI. M. OMARY	: Mwakilishi Mamlaka ya Masoko na Mitaji ya Dhamana
BI. A. KAALE	: Mwakilishi Mamlaka ya Masoko na Mitaji ya Dhamana
BW. B. KYANDO	: Mwakilishi wa CSD & Registry Company
BW. G. KAPANGE	: Mwakilishi wa CSD & Registry Company
BW. D. MWAKALINDILE	: Meneja wa Fedha TBL
BI. AMANDA WALTER	: Meneja Mawasiliano TBL

KUMB. NAMBA 1/2020 : KUSOMA TAARIFA YA MKUTANO

1.1. Katibu alisoma taarifa ya kuitishwa Mkutano Mkuu wa 47 wa Wanahisa wa kampuni ya Tanzania Breweries Public Limited Company, uliofanyika kwa njia ya mtandao kuanza saa nne kamili asubuhi.

KUMB. NAMBA 2/2020 : AKIDI YA MKUTANO

2.1. Katibu alithibitisha kupokea taarifa ya uwakilishi kutoka Kampuni ya AB InBev Africa B.V, (zamani SABMiller Africa B.V) ikimteua, Bw. Philip Redman kuiwakilisha katika mkutano mkuu wa 47 wa wanahisa.

2.2. Katibu alieleza kuwa kanuni ya 62 ya mwongozo wa uendeshaji wa kampuni inaelekeza kuwa akidi ya Mkutano Mkuu wa Wanahisa ni angalau wanahisa wawili wenye jumla ya asimilia 50

au zaidi ya hisa na mmoja wao anapaswa kuwakilisha kampuni ya AB InBev Africa B.V. Hivyo Katibu alithibitisha kuwa akidi ya Mkutano Mkuu wa 47 wa Wanahisa ilitimia.

KUMB. NAMBA. 3/2020 : AJENDA ZA MKUTANO

3.1. Ajenda ya mkutano ilikuwa;

(i) Taarifa ya kuitishwa kwa mkutano.

(ii) Kupitia na kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu uliopita

(iii) Yatokanayo na Mkutano Mkuu uliopita.

(iv) Kupitishaa Taarifa ya Fedha ya Mwaka na Ripoti ya Wakurugenzi katika kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba, 2019.

(v) Kuridhaia gawio la hisa lililolipwa katika mwaka wa fedha unaoishia Desemba 31, 2019.

(vi) Kuteua kampuni ya PricewaterhouseCoopers kama wakaguzi wa hesabu za Kampuni katika kipindi kinachoishia tarehe 31 Desemba, 2020.

(vii) Mengineyo

3.2. Ajenda ilithibitishwa.

KUMB. NAMBA. 4/2020 : KUPITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU ULIOPITA

4.1. Kumbukumbu za Mkutano Mkuu uliopita zilisomwa na kuthibitishwa kama kumbukumbu sahihi za Mkutano Mkuu uliopita.

KUMB. NAMBA 5/2020 : YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU ULIOPITA

Kufanya Mkutano Mkuu mapema

5.1. Iliarifiwa kuwa Menejimenti ilipanga kufanya Mkutano Mkuu wa Mwaka mapema kama ilivyokubaliwa na Wajumbe katika Mkutano Mkuu uliopita. Ingawa, mkutano ulichelewa kwa sababu ya kuzuka kwa janga la COVID-19, ambalo lilipelekea kuwepo vizuizi mbalimbali, ikiwemo zuio la mikusanyiko.

Uwakilishi wa wenye hisa chache katika Bodi ya Wakurugenzi

5.2. Wajumbe waliarifiwa kuwa Mwongozo wa kampuni ulibadilishwa ili kuruhusu wanahisa wenye hisa chache kwa umoja wao kuweza kuchagua wakurugenzi wawili kwenye Bodi ya Wakurugenzi. Rasimu ya tangazo lenye maelezo ya kina kuhusu sifa zinazohitajika zilitumwa kwa wanahisa. Uchaguzi wa kwanza ulitarajiwa kufanyika katika Mkutano

Mkuu wa Mwaka 2021. Wanahisa walihimizwa kuomba nafasi hizo wakati zitakapotangazwa.

Kubadilisha jina la kampuni

5.3. Iliarifiwa kuwa kufuatia idhini ya kubadilishwa kwa jina la kampuni kwenye Mkutano Mkuu uliopita, ombi lilishughulikiwa kupitia mfumo wa maombi kwa njia ya mtandao wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na jina la kampuni limebadilishwa kuwa Tanzania Breweries Public Limited Company, kuanzia Februari 2020. Wanahisa walihakikishiwa kuwa mabadiliko ya jina hayataathiri haki zao na kwamba vyeti vyao vya hisa au risiti za CDS, ambazo zina jina la zamani, zitaendelea kutumika.

Mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kimea Mkoani Dodoma

5.4. Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kilitoa hati ya motisha kwa kampuni kuwekeza katika kiwanda cha kutengeneza kimea Jijini Dodoma. Menejimenti ingefanya mawasiliano na Serikali kuomba motisha hiyo iboreshwe ili mradi uanze kutekelezwa.

5.5. Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuiafiki.

KUMB. NAMBA 6/2020 : KUTHIBITISHA TAARIFA YA MWAKA YA FEDHA NA RIPOTI YA WAKURUGENZI

6.1. Mwenyekiti aliwakaribisha Wajumbe katika Mkutano Mkuu wa 47 wa Wanahisa. Aliwaarifu kwamba mwaka wa fedha wa 2019 ulikuwa na changamoto mbalimbali, utendaji wa biashara kwa mwaka huo uliweza kuimarika ingawa ilikuwa katika mazingira tete. Faida ya uendeshaji ilikua kwa asilimia 5 zaidi ya mwaka uliotangulia, mapato ya TBLGroup katika kipindi hicho yalishuka kwa asilimia 5 ukilinganisha na mwaka uliopita. Hali hii ilitokana na kupungua kwa soko la bia wakati wa kipindi cha nusu ya pili ya mwaka, kutokana na kuyumba kwa kipato cha wateja ambayo iliwalazimu kuhamia kwenye pombe za gharama nafuu zaidi na hali mbaya ya hewa ikiwemo hatua ya kampuni kusitisha uzalishaji wa bia za asili.

6.2. Matokeo yake, mapato ya bia yalishuka kwa asilimia 4.6% wakati ya viywaji vya pombe kali na mvinyo yalishuka kwa asilimia 6.5% ikilinganishwa na mwaka uliopita. Licha ya

changamoto hizo, TBL Group iliweza kupata matokeo ya kutia moyo kutokana na kuongezeka mauzo ya bia ya Castle Lite na Safari Lager. Faida kwa kipindi hicho ilikuwa shilingi bilioni 220 na jumla ya gawio la shilingi bilioni 147 zililipwa kwa wanahisa (shilingi 500 kwa kila hisa).

6.3. TBL Group iliendelea kuwa moja ya walipa kodi wakubwa nchini na kuchangia kwa kiasi kikubwa mapato ya Serikali kupitia malipo ya kodi ya mapato, kodi ya ushuru wa bidhaa na kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na kodi ya kampuni. Jumla ya shilingi bilioni 466 zililipwa katika kipindi hicho cha mwaka.

6.4. TBL Group pia iliendelea kusaidia jamii kote nchini kupitia mpango wake wa Uwajibikaji kwa Jamii (CSR), uliolenga kusaidia wakulima na kununua malighafi ya ndani. Katika jitihada za kuwapatia ujuzi, kuwaunganisha na kuwawezesha kupata huduma za kifedha, TBL ilizindua Programu ya KilimoUza ambayo ilikuwa jukwaa kubwa la kuwawezesha kupata ujumbe wenye taarifa mbalimbali kupitia simu zao za mkononi kwa mfumo wa USSD unaowaunganisha wakulima wa shayiri na kuwasaidia kupata habari muhimu kwa kufanya maamuzi kuhusu kilimo.

6.5. Kampuni ilifanikisha dhamira yake ya kuongeza matumizi ya malighafi kutoka ndani kama mshirika muhimu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Tanzania. Kwa mwaka mzima, ilinunua asilimia74 ya malighafi (yenye thamani ya shilingi bilioni 130). Malighafi hizo ni pamoja na shayiri, mahindi, mtama na zabibu kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa zake. Kwa kuongezea, TBL Group iliendelea kutumia jukwaa la #ISIWESABABU kutoa elimu na kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia, kuchochea mazungumzo ambayo yanakuza uhusiano mzuri na tabia njema katika jamii.

6.6. Mwenyekiti alieleza hatua zilizochukuliwa katika kupambana na changamoto ya ugonjwa wa UVIKO (COVID-19). Alisema kuwa janga hili lilileta changamoto ambazo hazijawahi kutokea kwa jamii, Serikali, na wafanyabiashara kote ulimwenguni na nchini Tanzania. zilichukua hatua tofauti kulinda watu wao na uchumi. Vitendo hivi vilikuwa na athari tofauti kwa biashara na uwezo wao wa kufanya kazi. Alipongeza hatua za Serikali ya Tanzania za kukabiliana na janga hilo kwa kuweka uchumi wazi na kuruhusu biashara kuendelea na watu kufanya kazi huku ikisisitiza umuhimu wa kujikinga na kuchukua tahadhari.

6.7. Katika kukabiliana na janga la UVIKO (COVID-19), TBL ilitoa kipaumbele zaidi kwa afya na usalama wa wafanyikazi wake. Hatua kadhaa zilichukuliwa kuweka mazingira salama ya kufanyia kazi. Pia, kampuni ilizalisha na kutoa msaada wa vitakasa mikono na vifaa vya kinga binafsi (PPE) kwa wafanyikazi wake, kwa serikali na makundi mbalimbali ya jamii. Pia ilitoa elimu kwa wateja katika baa, kwa njia ya mtandao na kupitia vyombo mbalimbali vya habari, kusambaza vifaa vya kinga na kutoa ushauri kwa wenye mabaa juu ya jinsi ya kuendelea kufanya kazi kwa usalama.

6.8. Kampuni iliamua kubana matumizi kwa kupunguza gharama na kuhakikisha mzunguko wake wa pesa unaendelea. Hatua hizi zilichukuliwa ili kuhakikisha biashara inaweza kustawi, na kutumia fursa ambazo zingetokea kutokana na janga la ugonjwa huu.

6.9. Alisema kuwa katika kipindi kifupi biashara iliathiriwa na janga hilo la Kidunia, alifurahi kuona jinsi hali ilivyoanza kuimarika tena kwa haraka na aliamini kuwa ingeendelea na kukua. Usimamizi ulibaki kulenga kuongoza kufufua na kurudisha biashara kwenye ukuaji, na uangalifu endelevu juu ya ufanisi wa gharama, kusaidia uwekezaji wa ubunifu wa bidhaa mpya, huku ikijenga uwezo wa wafanyikazi wake kufanikisha ukuaji endelevu.

6.10. Alishukuru wateja kwa kuendelea kuziamini bidhaa za kampuni na kuendelea kuiunga mkono kampuni yao na akawashukuru viongozi na wafanyakazi kwa kujitolea na kuendesha biashara kufikia kiwango ilichofika na kuiweka katika mazingira mazuri ya ukuaji kwa siku zijazo. Aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuweka mazingira mazuri ya biashara kwa TBL Group na viwanda vingine kuendelea kustawi.

6.11. Wajumbe walipitia na kupitisha Taarifa ya Mwaka ya Fedha na Ripoti ya Wakurugenzi.

KUMB. NO. 7/2020: KUIDHINISHA GAWIO LILILOLIPWA KWA MWAKA ULIOMALIZIKA 31 DESEMBA 2019

7.1. Azimio la kuthibitisha wa malipo ya Tsh 500.00 kama gawio kwa kila hisa kwa mwaka ulioishia 31 Desemba 2019 liliwasilishwa.

7.2. Wajumbe walilipokea na kuthibitisha malipo ya gawio la Tsh. 500.00 kwa kila hisa yaliyolipwa kwa mwaka ulioishia 31 Desemba 2019.

KUMB. NO. 8/2020: UTEUZI WA KAMPUNI YA UKAGUZI WA HESABU

8.1.Wakurugenzi walipendekeza uteuzi wa Kampuni ya PricewaterhouseCoopers kama wakaguzi wa nje wa hesabu za Kampuni kwa mwaka unaoishia 31 Desemba 2020.

8.2.Wajumbe walilipokea na kuidhinisha uteuzi wa kampuni ya PricewaterhouseCoopers kama wakaguzi wa nje wa hesabu za Kampuni kwa mwaka unaoishia 31 Desemba 2020.

KUMB. NO. 9/2020: MENGINEYO

9.1.Wanahisa wenye maswali au wanaohitaji ufafanuzi wa jambo lolote la kiutawala waliombwa kuwasiliana na uongozi kwa kutuma barua pepe katika Kitengo cha Mawasiliano cha TBL.

KUMB. NO. 10/2020: KUFUNGA MKUTANO

10.1. Mwenyekiti aliwashukuru wanachama kwa michango yao mizuri ya mawazo wakati wa mkutano.Alifunga mkutano saa 4:50 asubuhi.

ZIMETHIBITISHWA: ----------

MWENYEKITI

TAREHE : ----------

TANZANIA BREWERIES PUBLIC LIMITED COMPANY

MKUTANO MKUU WA 47 WA WANAHISA

MAHUDHURIO

1.	BERNARD GRISEL	MJUMBE
2.	EVE KENNEDY	MJUMBE
3.	PETER KISINGA	MJUMBE
4.	GABRIEL BUJULU	MJUMBE
5.	LAWRENCE GONZALES	MJUMBE
6.	WINGRACE GERALD	MJUMBE
7.	J. KILAMA	MJUMBE
8.	SHARIFA ISSA	MJUMBE
9.	ANDREW MGUNDA	MJUMBE
10.	HADIJA MWINYI	MJUMBE
11.	TANZANIA SECURITIES LTD	MJUMBE
12.	SPORT GUCHA	MJUMBE
13.	DENIS DEOGRATIAS	MJUMBE
14.	JACOB BWANATUMBO	MJUMBE
15.	JUMA RUMONDO	MJUMBE
16.	LOUIS COLACO	MJUMBE
17.	MELVIN K	MJUMBE
18.	MWANSWASWA F. NSOLO	MJUMBE
19.	NANA TEMU	MJUMBE
20.	NEEMA HASSAN	MJUMBE
21.	NISHIT LADWA	MJUMBE
22.	PERFECTUS JOSEPH URIO	MJUMBE
23.	PETER MOSHY	MJUMBE
24.	A. MBILIKIRA	MJUMBE
25.	AZIM HOODA	MJUMBE
26.	ERICA SANGA	MJUMBE
27.	BRIAN CHUWA	MJUMBE
28.	GODFREY MASHAURI	MJUMBE
29.	GRACE SAGUTI	MJUMBE
30.	MARIAM MAHIGE	MJUMBE
31.	MARGARETH MARTIN	MJUMBE
32.	MKUNDE MLAY	MJUMBE
33.	NANCY ABRAHAM	MJUMBE
34.	NGEMERA NDIBALEMA	MJUMBE
35.	OMBENI	MJUMBE
36.	LAWRENCE SAGUTI	MJUMBE
37.	JACQULINE KILAMA	MJUMBE
38.	AISHA MBILIKIRA	MJUMBE
39.	WIVINA MUSHOBOZI	MJUMBE
40.	JOHN NKANE	MJUMBE
41.	MICHAEL OROTTA	MJUMBE